

Nchi za Ulaya zinazofanya kazi kwa pamoja

# KUOMBA HIFADHI, KUTAFUTA FAMILIA NA KUHAMA

→ Ikiwa unataka **kuomba hifadhi** kwa sababu nchi yako si salama kwako, wajulishe maafisa hao. Mamlaka **husika itakusajili.**


**Baki katika nchi ambamo umesajiliwa.**

## WAKATI WA USAJILI, MAAFISA HAO WATA

- Kuuliza jina lako, umri na uraia. Pia watakuuliza kuhusu familia yako na jinsi ulivyofika hapa.
- Watapiga picha yako na kuchukua alama za vidole (kuanzia watoto wenye umri wa miaka 6 na zaidi).
- Watakagua hati zako (Kitambulisho, pasipoti, cheti cha kuzaliwa) na kukuomba taarifa zako za mawasiliano.

## WAAMBIE MAAFISA HAO IKIWA

- Una umri chini ya miaka 18 na umewasili peke yako. Watamteua mtu anayeitwa mlezi kukusaidia.
- Kutafuta familia yako. Watakusaidia kuwapata ikiwa ni kwa maslahi yako bora. Zungumza na mlezi wako, ikiwa hutaki kungana na familia yako.
- Unaifahamu nchi yoyote ya Ulaya kwa sababu ulikuwa huko hapo awali.
- Huhisi vizuri au una wasiwasi kuhusu jambo fulani.




Ikiwa watu wengi sana watafika kwa wakati mmoja katika nchi hii, baadhi yao wanaweza **kuhamishwa kwenda nchi nyingine ya Ulaya.**

Huwezi kuchagua nchi **utakayopelekwa.**

**Unaweza kukata rufaa** ikiwa hukubaliani na wewe kuhamishwa lakini ni lazima ueleze sababu.

## KUMBUKA

- Unaweza daima kuomba wakili ili kupata ushauri
- Omba mkalimani ikiwa huzungumzi lugha hiyo.
- Kila mtu anayefanya kazi hapa lazima akuhudumie kwa heshima.
- Shirikiana na maafisa hao. Waombe waeleze wanachomaanisha ikiwa jambo lolote wanalosema halieleweki.



© Shirika la Umoja wa Ulaya wa Masuala ya Hifadhi, 2025

euaa
EUROPEAN UNION AGENCY FOR ASYLUM